


Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 03 Issue: 01 | April-2024

EAJK

# Uchanganuzi wa mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya kwa misingi ya michepuo ya masomo

**Author**
**Jackson Mutuku Kavoi**
**Email:** jkavoi@kabarak.ac.ke

**Chuo Kikuu cha Kabarak, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Kavoi, J. M. (2024). Uchanganuzi wa mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya kwa misingi ya michepuo ya masomo. *East Africa journal of Kiswahili*, *3*(1), 8-21. https://doi.org/10.51317/eajk.v3i1.484

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 29.02.2024
Accepted: 21.03.2024
Published: 01.04.2024

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2024 by the author(s). This article is an open access article distributed under the license of the Creative Commons Attribution (CC BY NC SA) and their terms and conditions.

**Ikisiri**
Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua mielekeo ya wanafunzi wa kozi za sayansi na sanaa kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili nchini Kenya. Aidha, kuchunguza visababishi vya mielekeo husika kuhusu umuhimu wa matumizi ya Kiswahili kufundisha stadi za mawasiliano. Muundo wa Uchunguzi Kimaelezo ulitumiwa, huku taasisi 5 za kiufundi za kitaifa na sampuli ya wanafunzi 148 wakishirikishwa katika utafiti. Fomula ya Balian (1988) ya uteuzi wa sampuli ilizingatiwa na ukusanyaji wa data ulitumia kitanga cha mielekeo ya hojaji ya Likert kilichokarabatiwa, maswali ya wazi na dodoso. Waaidha, Zanatepe ya Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii (*SPSS*) kilitumika kuchanganua data. Matokeo yalidhihirisha kuwa, asilimia 2.82 ya wanafunzi 142 waliohusishwa katika uchanganuzi walidhihirisha mielekeo hasi, ilhali asilimia 97.18 walionyesha mielekeo chanya kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi nchini Kenya. Aidha, wanafunzi wa kozi za sanaa walidhihirisha mielekeo chanya ya chini wakilinganishwa na wenzao wa sayansi. Uchanya huu ulitokana na faida ya utoaji wa huduma uwandani kwa wateja wao waliyoiambatanisha na kuridhia Kiswahili kitumike katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano. Kwa mkabala huu, wanafunzi wa taasisi husika waliona umuhimu wa mawasiliano kabambe katika utoaji huduma nyanjani. Hivyo, kuanzishwa kwa ufundishaji wa stadi za mawasiliano kwa kutumia Kiswahili sambamba na Kiingereza kungewasaidia kuchonga maarifa yaliyogusia mawasiliano. Matokeo ya utafiti huu ni ya umuhimu kwa Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala, Kenya katika utungaji wa sera ya elimu katika taasisi husika.

**Maneno muhimu:** Kiswahili, michepuo, mielekeo, stadi za mawasiliano, wanafunzi wa taasisi za kiufundi.

## UTANGULIZI

Stadi za Mawasiliano ni somo ambalo hujihusisha na mikakati ya uondoshaji wa vizuizi vya mawasiliano miongoni mwa wawasilianaji. Katika taasisi yoyote ambayo inalenga kufikia matokeo bora, hutathimini mahusiano miongoni mwa wafanyakazi wake na jinsi ya kuboresha mahusiano husika. Kwa mkabala huu, stadi za mawasiliano zimekubalika katika tasnia mbalimbali zinazojihusisha na utoaji wa huduma, hususani tasnia ya tiba, hasa katika elimu tiba. Kuhusiana na hili, tafiti mbalimbali kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa tiba kuhusu Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza katika kiwango cha chuo kikuu zimefanywa. Kwa mfano, tafiti za Lumma-Sellenthin (2012), Rees na Sheard (2002) miongoni mwa nyingine. Hata hivyo, tafiti zinazoshirikisha lugha nyingine, hususani Kiswahili hazijafanywa kwa undani. Kwa usahili kabisa, Eagly na Chaiken (1993) anajeleza mielekeo kama "hali ya kisaikolojia inayopambanuliwa kwa kutathmini kitu fulani kwa hali ya kukipenda au kukikataa" (uk. 1). Kitu husika kinaweza kuwa ni lugha ya mhusika au lugha ya wengine au kitu fulani. Kwa hali hii, mielekeo ni kigezo muhimu kwani hushawishi jinsi watu wanavyoitikia kuhusu mtu binafsi, lugha au kitu. Kwa mfano, tafiti kadha zimeibua jinsi mielekeo na umotishaji huchangia katika upataji wa lugha ya pili (Lightbown & Spada, 1993). Kimsingi, mielekeo hutathmini jinsi watu huhusisha thamani kuhusu mtu, lugha, taasisi au kitu fulani. Mielekeo pia huathiri tabia ya mhusika kwa namna moja au nyingine, huku kichocheo chake kikidhihirisha matokeo ya faida au hasara; ndiposa Mohochi (2005) anasema binadamu hujenga mielekeo chanya au hasi kulingana na manufaa au hasara kwa chombo husika.

Katika tafiti tangulizi iligunduliwa kuwa mielekeo inaweza kuathiri uitikiaji wa kupenda au kutopenda jambo ama kitu fulani. Kwa hali hii, mielekeo ina nafasi muhimu ya kuathiri ujifunzaji na ufundishaji wa lugha. Mbali na lugha, mielekeo inaweza kuathiri mambo mengine mengi, likiwemo ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Kwa sasa somo hili hufundishwa kwa Kiingereza kwa azma ya kuwasaidia wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuboresha mawasiliano yao vyuoni na kuwasiliana na umma wanapoenda nyanjani kuihudumia. Hata hivyo, hali halisi ni kuwa wanaoenda kuhudumia umma nyanjani hutangamana na umma ambayo ufahamu wayo wa Kiingereza ni finyu mno au haikijui hata kidogo. Hivyo, hawa hukumbana na kikwazo cha mawasiliano ambacho kingeweza kuondolewa kupitia ufundishaji wa somo la Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi hizi. Lugha ya Kiswahili inafahamika kwa asilimia zaidi ya 85 ya watu nchini Kenya, na hufanya msingi ufaao wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Hata hivyo, suala la mielekeo kuhusu ufundishaji wa stadi za mawasiliano kwa ujumla wake, mbali na ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili, halijatafitiwa kikamilifu. Hivyo basi, ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu ulichanganua na kubainisha mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Katika kuhakiki maandishi yanayogusia madhumuni tafitiwa, yanajikita katika sehemu tatu: maandishi yanayohusiana na mielekeo ya lugha kwa ujumla na baadaye tafiti zinazogusia mielekeo ya lugha ya Kiswahili. Halikadhalika, maandishi yanayoangazia mielekeo kuhusu stadi za mawasiliano.

Dhana hii inapotumika katika nyanja za kiusomi huhusishwa na hali ya kupendelea au kutopendelea kitu, jambo au hata hali fulani. Alhmali (2007) anasema kwamba watafiti katika nyanja za kisaikolojia na elimujamii, na hasa katika ujifunzaji wa lugha, waliibua vijelezi kadhaa vya mielekeo ambavyo hufafanua maana tofauti katika miktadha mbalimbali. Mills (1998) anafasili mielekeo kama hali ya kifikra au hisia kuhusu mtu au hali fulani. Maoni haya yanaoana na ya Katz (1960) anayefafanua mielekeo kuwa hali ya mtu kutia jambo au kitu katika mizani na kuibuka na maamuzi ya kukipenda au kukichukia. Naye, Padwick (2010) ana maoni kuwa licha ya mtazamo wa kiakili wa kupenda au kutopenda kujifunza lugha fulani, mtu huathiriwa na masuala ya kisaikolojia na kijamii. Kimsingi, jinsi mtu anavyoitikia hutegemea zaidi hamasa na mielekeo ya anayejifunza lugha lengwa. Maoni ya Padwick yanakaribiana na ya Gardner na Lambert (1972) ambao wanahitimisha kuwa uwezo wa mtu katika ujifunzaji wa lugha ya pili huathiriwa na umilisi wa kiakili au ujuzi

wa lugha. Pia, hutegemea mielekeo na mitazamo yao kuhusu lugha lengwa. Vivyo hivyo, mielekeo ni "mtazamo wa ndani wa mtu kuhusu kitu, jambo au hali fulani" (Nyandwaro, 2015). Kwa hali hii, kama mwanafunzi wa taasisi ya kiufundi ya kitaifa angekuwa na mwelekeo chanya kuhusu Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili, angezikaribisha kwa njia ya kuzipendelea na ikiwa angekuwa na mwelekeo hasi kuzihusu, basi angeitikia kwa njia ya kuzichukia. Kwa kawaida, stadi za mawasiliano zikiwa na maana ya zana zinazotumiwa kuondosha vikwazo vya mawasiliano kabambe ambazo hujumuisha stadi za lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika) na viziada lugha kama ishara, mawasiliano miondoko au jicho mtagusano (Wanjala & Kavoi, 2013).

Fazel na Aghamolaei (2011) alitathmini mielekeo ya wanafunzi wa utabibu katika Chuo Kikuu Hormozgan kuhusu ujifunzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza na matokeo yake yalidhihirisha kuwa palikuwa na tofauti ya kimielekeo kati ya wanafunzi wa sayansi asilia na wa utabibu sayansi. Ulinganishi unapofanywa, inagundulika kuwa wanafunzi wa sayansi asilia walidhihirisha mielekeo chanya ya juu kuhusu stadi za mawasiliano wakilinganishwa na wanafunzi wa utabibu sayansi. Ingawa utafiti wao unafanana na utafiti huu, michepuo ya masomo yao, ambayo ni sanaa na sayansi yalikuwa tofauti, hivyo kudhihirisha matokeo tofauti ya kimielekeo hali inayoshajiisha kufanyika kwa utafiti huu. Aidha, Trifkovc et al. (2017) walifanya utafiti wa wanafunzi wa uuguzi wa Chuo Kikuu cha Mozibor na kugundua kuwa palikuwa na tofauti ya kimielekeo ambapo wanafunzi wa mwaka wa pili walidhihirisha mielekeo chanya ya juu ikilinganishwa na wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Japo utafiti huu unafanana na utafiti huu, ni tofauti katika lugha iliyotumika katika ujifunzaji wa stadi za mawasiliano na michepuo ya masomo na programu lengwa. Tafiti nyingine ambazo zimeshughilikia mada tafitiwa ni: Al-Bizrah et al. (2016), Alotaibi na Alsaeed (2016), Karin et al. (2017), Neupane et al. (2012) na Rees na Sheard (2002) miongoni mwa wengine. Baada ya kutathmini tafiti hizi, ni wazi kuwa zilihusisha wasailiwa kutoka wanatiba; wote kutoka vyuo vikuu. Kwa upande mwingine, utafiti huu ulijihusisha na wasailiwa kutoka taasisi za kiufundi katika mwaka wao wa nne kiwango cha stashahada katika mchepuo ya sayansi na sanaa, mwaka wa mwisho wa masomo. Pia, tafiti tangulizi zilifanyika katika vyuo vikuu, ilhali utafti huu ulifanyika katika taasisi za kiufundi za kitaifa.

**MBINU ZA UTAFITI**

Muundo wa Uchunguzi wa Kimaelezo ulitumika katika utafiti huu ambapo hueleza na kufafanua matukio kama yalivyo, yalivyokuwa au yatakavyokuwa (Oso & Onen, 2005). Muundo huu ulipendelewa kwa sababu ulisaidia kubuni maswali ambayo yaliibua data iliyokuwa ikihitajika (Kombo & Tromp, 2006). Kigeu cha kidemografia ambacho ni michepuo ya masomo kilichanganuliwa ili kufanikisha madhumuni ya utafiti huu.

Utafiti huu uliendeshwa katika taasisi tano za kiufundi za kitaifa nchini Kenya ambazo ziliteuliwa kinasibu. Wasailiwa 148 waliteuliwa kinasibu kutoka taasisi hizi na kozi zenye mketo wa utoaji wa huduma vijijini. Wasailiwa hawa walijumuisha wanafunzi wa mwaka wa pili wa astashahada na mwaka wa tatu wa stashahada waliokuwa wakimaliza masomo yao. Wasailiwa waliotumika katika uchanganuzi walikuwa 142.

Utafiti huu ulitumia hojaji iliyokarabatiwa kutoka Kitanga cha Kupimia Mielekeo kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza kilichobuniwa na Rees et al. (2002) na nyongeza ya kauli chache kutoka kwa mtafiti (kauli 24 zilitumika). Kabla ya kwenda uwandani kwa ukusanyaji data, utafiti wa awali uliendeshwa ambapo kauli teule zilipitishwa kwa Zanatepe ya Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii (*SPSS* Toleo la 23) ili kuchanganua kizidishi cha uthabiti (*coefficient reliability*). Kimaudhui na kimajibu, maswali ya wazi yalidhihirisha uthabiti, jambo ambalo lilidhihirisha yalikuwa yamefikia utegemeo wa hali ya juu; hivyo kufaa katika ukusanyaji wa data katika utafiti halisi. Katika utafiti wa kimielekeo, uhalali wa kauli katika hojaji huhitajika kudhihirika kupitia kwa wataalamu wa kisaikolojia (Anvik et al., 2007); ambao ulitekelezwa.

Waaidha, Zanatepe ya Kichanganuzi Data ya Kitakwimu za Sayansi Jamii (*SPSS* Toleo la 23) ilitumika katika uchanganuzi wa data ili kufikia madhumuni ya utafiti. Kutoka *SPSS*, ANOVA-njia moja na uthibitisho zaidi ulitolewa kupitia *t-test* huru sampuli mbili. Matokeo yaliyokokotolewa yalitumiwa kubainisha uhusiano uliopo wa kimielekeo na matumizi ya Kiswahili katika ufundishaji wa stadi za mawasiliano. Uwasilishaji wa data ulitumia grafu mihimili na majedwali.

**UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO**

**Sifa za Kidemografia za Wasailiwa Wanafunzi**

Utafiti huu ulishirikisha wasailiwa wanafunzi 148. Hata hivyo, walioshirikishwa katika uchanganuzi wa data walikuwa 142. Hali hii ilitokana na wasailiwa 6 walioshiriki katika ujazaji wa hojaji, kutozikamilisha, ilivyohitajika, hivyo hazikuwa na umuhimu wowote katika uchanganuzi wa data. Hivyo, uitikiaji wa ujazaji wa hojaji ulikuwa asilimia 95.95 (n=142). Jedwali 1 linalofuata linawasilisha sifa za wasailiwa wanafunzi walioshirikishwa katika utafiti huu.

**Jedwali 1: Sifa za Kidemografia za Wanafunzi wa Taasisi za Kiufundi za Kitaifa**


| Sifa (Umri, Michepuo) | Idadi (n) ya Wasailiwa | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| **Umri** | | |
| **< 20** | 20 | 14 |
| **20-25** | 107 | 77 |
| **26-30** | 10 | 7 |
| **31-35** | 1 | 1 |
| **>35** | 1 | 1 |
| **Michepuo ya Masomo** | | |
| **Sayansi** | 73 | 51.41 |
| **Sanaa** | 69 | 48.59 |

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)

Kwa mujibu wa Jedwali 1, wanafunzi waliokuwa wakisoma kozi zenye mwegemeo wa sayansi walikuwa asilimia 51.41 (n=73), ilhali wa sanaa walikuwa asilimia 48.59 (n=69). Msambao huu wa wasailiwa kimichepuo unatokana na hali kuwa wanafunzi wa sanaa ni wachache kuliko wa sayansi na kwa kawaida taasisi za kiufundi huwa zina mwegemeo wa masomo ya sayansi.

**Msambao wa Kozi mbalimbali zilizotumika katika Utafiti**

Ili kufanikisha malengo ya utafiti huu, kozi ambazo zilikuwa zikiegemea michepuo ya sanaa na sayansi; zenye mketo wa utoaji huduma zilichaguliwa. Kozi zilizoegemea sanaa zilizoshirikishwa katika utafiti huu ni Usimamizi wa Biashara, Mauzo na Masoko, Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii, Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, Ununuzi na Usambazaji, Usimamizi wa Msururu wa Usambazaji na Usimamizi wa Wafanyakazi. Kwa ujumla, kozi zenye mketo wa sanaa zilikuwa saba (7). Kwa upande wa sayansi, ulishirikisha Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu, Teknolojia Sayansi ya Maabara, Kilimo cha Kawaida, Ufundi wa Umeme, Mitindo ya Nguo na Ushonaji na Ususi na Tiba ya Urembo ambazo zilikuwa sita (6). Kwa ujumla, kozi zote zilikuwa kumi na tatu (13). Fauka ya haya, kozi zote ziliegemea utoaji wa huduma vijijini. Mchoro 1 ufuatao unawasilisha wasailiwa wa kozi husika na idadi iliyoshirikishwa katika utafiti.




**Mchoro 1: Msambao wa Kozi mbalimbali zenye Mwegemeo wa Utoaji Huduma**
Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)

Wasailiwa wakilishi katika kozi mbalimbali waliteuliwa kulingana na idadi ya wanafunzi katika kila kozi. Kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii ilikuwa na asilimia 21.83 (n=31), ikifuatiwa kwa karibu na kozi ya Ufundi wa Umeme kwa asilimia 19.72 (n=28). Kozi nyingine zenye wasailiwa kiasi, zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika yenye asilimia 14.08 (n=20) na Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu ikiwa na asilimia 11.27 (n=16). Hizi na nyingine zenye idadi wastani zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Msururu wa Usambazaji, asilimia 8.4 (n=12) na Kilimo cha Kawaida asilimia 9.86 (n=14). Kozi ambazo zilishirikisha idadi ndogo ya wasailiwa zilikuwa ni pamoja na Usimamizi wa Biashara, asilimia 2.82 (n=4); Mauzo na Masoko, asilimia 2.11 (n=3); Ununuzi na Usambazaji, asilimia 1.41 (n=2) na Usimamizi wa Wafanyakazi, asilimia 1.41 (n=2) kwa upande wa sanaa. Kwa upande wa sayansi, kozi wakilishi zenye wasailiwa wachache zilikuwa ni Teknolojia Sayansi ya Maabara, asilimia 4.23 (n=6); Mitindo ya Nguo na Ushonaji, asilimia 1.41 (n=2) na Ususi na Tiba ya Urembo, asilimia 1.41 (n=2).

Msambao wa wasailiwa waliotumika katika utafiti huu unaendana na idadi ya wanafunzi katika taasisi za kiufundi za kitaifa. Kutokana na data husika, inaonekana kuwa baadhi ya kozi ni maarufu kuliko nyingine na hivyo kuvutia wanafunzi wengi. Kwa mfano, kozi ya Huduma za Jamii na Ustawi wa Jamii (21.83%), Ufundi wa Umeme (19.72%), Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (14.08%) na Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu (11.27%), zikilinganishwa na idadi ndogo katika kozi nyingine kama Mitindo ya Nguo na Ushonaji (1.41%) na Ususi na Tiba ya Urembo (1.41%). Sehemu

inayofuata inajikita katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti.

**Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Matumizi ya Kiswahili Kufundishia Stadi za Mawasiliano**

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni yaliyolenga kutathmini mielekeo ya wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano. Mielekeo ya wanafunzi ilipimwa kwa kuzingatia kauli za hojaji ya Likert iliyokarabatiwa kutoka Kitanga cha Rees et al. (2002) pamoja na mtafiti. Kama ilivyotangulizwa kusemwa katika utafiti huu, kauli zote kwa ujumla zilikuwa 24; zenye uchanya zikiwa 13 na zenye uhasi zikiwa 11. Jedwali 2 linalofuata linadhihirisha msambao wa idadi ya kauli zilizotumika.

**Jedwali 2: Msambao wa Idadi ya Kauli**

| Vijenzi vya Mielekeo | Kauli | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Chanya | Hasi | |
| Fikra | 5 | 4 | 9 |
| Hisia | 5 | 5 | 10 |
| Vitendo | 3 | 2 | 5 |
| Jumla | 13 | 11 | 24 |

Chanzo: Data kutoka Uwandani (2017)

Kwa ujumla, kauli chanya ni 13, ilhali kauli hasi ni 11. Zaidi ya haya, kauli hizi zinagawanywa kwa kigezo cha vijenzi vya mielekeo: fikra chanya 5, hisia chanya 5, na vitendo chanya 3. Kauli hasi, nazo, zinagawika katika fikra hasi 4, hisia hasi 5 na vitendo hasi 2.

**Mielekeo ya Wanafunzi ya Kijumla kuhusu Ufundishiji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili**


Kwa ujumla, mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano ilikuwa chanya. Baada ya uchanganuzi wa data, taasisi za kiufundi za kitaifa zilidhihirisha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundisha Stadi za Mawasiliano. Jedwali 3 linalofuata linatoa muhtasari wa matokeo ya uchanganuzi husika ambapo Kabete National Polytechenic (KANAPO) ilikuwa na alama ya wastani 80.94, Kenya Coast National Polytechnic (KECONAPO) 87.79, Kisii National Polytechnic (KINAPO) 85.26, Meru National Polytechnic (MENAPO) 87.75 na The Eldoret National Polytechnic (TENAPO) 86.16. Hata hivyo taasisi zote zilidhihirisha mielekeo chanya kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano kama inavyodhihirika katika Jedwali 3.

**Jedwali 3: Alama ya Mielekeo ya Wastani kwa Taasisi zote**

| TAASISI YA KIUFUNDI | MIELEKEO CHANYA (ALAMA) | MIELEKEO YA UKATIKATI (ALAMA) | MIELEKEO HASI (ALAMA) |
|---|---|---|---|
| Kabete | 81.03 | 0.00 | 66.50 |
| Kenya coast | 87.79 | 0.00 | 0.00 |
| Kisii | 85.26 | 0.00 | 68.00 |
| Meru | 87.79 | 0.00 | 0.00 |
| The Eldoret | 86.16 | 0.00 | 0.00 |

Chanzo: *SPSS* toleo 23, (2017); Data Iliyochanganuliwa

Zaidi, Mchoro 2 unawasilisha zaidi alama za wastani za mielekeo kwa kila taasisi ya kiufundi ya kitaifa.




**Mchoro 2: Alama za Wastani kwa Taasisi za Kiufundi za Kitaifa**

Waaidha, alama ya wastani ya mielekeo inadhihirishwa katika Jedwali 4 ambapo alama ya wastani ya mielekeo ya wanafunzi katika taasisi zote ilikuwa 85.31. Hata hivyo, alama ambayo ilikuwa kigezo cha maamuzi ya uchanya au uhasi wa mielekeo iliteuliwa kwa kuzingatia alama za jumla za kila msailiwa ambazo hatimaye zilidhihirisha maoni ya kila msailiwa. Kwa mfano, ikiwa hojaji ilikuwa na kauli ishirini na nne (24), kama ya utafiti huu, alama zifuatazo zilijidhihirisha: 24×5=120 (uitikiaji wa juu kabisa); 24×3=72 (uitikiaji wa uvuguvugu) na 24×1=24 (uitikiaji wa chini kabisa). Hivyo basi, alama za wastani kwa kila msailiwa mwanafunzi zilikuwa kati ya 24 na 120. Ikiwa alama kwa msailiwa zilikuwa juu ya 72, zilidhihirisha uchanya na ikiwa zilikuwa chini ya 72, uhasi ulikuwa umedhihirika. Alama 72 zilidhihirisha kwamba msailiwa alikuwa hajafanya maamuzi yoyote (Kothari, 2004; Mcleod, 2008). Hivyo, alama tarajiwa ya chini ikiwa 24 na ya juu ikiwa 120. Kwa mkabala huu alama ya wastani inayodhihirisha ukatikati ikiwa 72. Kwa hali hii, ikiwa alama ya wastani ni zaidi ya alama ya ukatikati 72, basi inamaanisha mielekeo ya wanafunzi ni chanya na ikiwa ni chini ya alama ya ukatikati 72 inamaanisha mielekeo ni hasi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano. Alama ya mielekeo ya chini=24; Alama ya mielekeo ya ukatikati=72; Alama ya mielekeo ya juu=120. Jedwali 4 linalofuata linaelezea haya kwa muhtasari.

**Jedwali 4: Alama ya Wastani ya Mielekeo ya Wanafunzi wa Taasisi za Kiufundi**

| Kigeu | Idadi ya Wasailiwa | Alama Wastani | Achano Sanifu | Alama ya Chini | Alama ya Ukatikati | Alama ya Juu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Alama** | 142 | 85.31 | 9.00 | 24 | 72 | 120 |

Chanzo: *SPSS* toleo 23, (2017); Data Iliyochanganuliwa

Kuhusiana na matokeo haya, Alotaibi na Alsaeed (2016) alipofanya utafiti kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa tiba katika Chuo Kikuu cha Taif, kuhusu ujifunzaji wa stadi za mawasiliano kwa Kiingereza, aligundua kuwa mielekeo yao ilikuwa ya uchaya wa juu. Hali hii pia ilidhihirika katika utafiti wa Richa, Yashoda &

Puranik (2017) alipogundua kuwa wanafunzi wa Mji wa Bengaluru, India mielekeo yao ilikuwa chanya kuhusu wao kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza. Waliandikisha alama za mielekeo chanya 50.44 na hasi 29.77. Hivyo asilimia 96.8 walikaribisha Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza katika mtaala wao wa masomo. Vivyo hivyo, wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya kama wenzao wa Bengaluru waliridhia kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili ili waweze kuhudumia wateja wao ipasavyo baada ya kufuzu.

**Mielekeo ya Wanafunzi kwa Misingi ya Michepuo ya Masomo**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kuchanganua mielekeo ya wanafunzi wa michepuo ya kozi za sanaa na sayansi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano. Wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya katika kusoma taaluma tofautitofauti hujiunga na kozi mbalimbali. Kozi hizi huwa katika michepuo miwili: sanaa na sayansi. Ili kufanikisha utafiti huu, kozi ambazo zilikuwa zinaegemea katika utoaji wa huduma, na hasa katika sehemu za vijijini, zilichaguliwa. Kozi teule zenye mketo wa sanaa zilikuwa ni Huduma za Jamii na Ustawishaji Jamii, Usimamizi wa Biashara, Mauzo na Masoko, Usimamizi wa Vyama vya Ushirika, Usimamizi wa Msururu na Usambazaji, Ununuzi na Usambazaji, na Usimamizi wa Wafanyakazi. Kozi zilizoegemea sayansi zilikuwa ni Ufundi wa Umeme, Kilimo cha Kawaida, Mitindo ya Nguo na Ushonaji, Teknolojia ya Vipimo vya Matibabu, Teknolojia Sayansi ya Maabara, na Ususi na Tiba ya Urembo. Kozi hizi ziliegemea utoaji wa huduma. Ili kufikia lengo la utafiti huu, swali ***"wanafunzi wa kozi za sanaa na sayansi katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya, wana mielekeo ipi kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili?"*** lilipaswa kujibiwa.

Jibu la swali hili lilipatikana kwa kutumia kichanganuzi cha ANOVA-njia moja ili kukokotoa tofauti ya kimielekeo ya wanafunzi kwa kuzingatia kigeu cha michepuo ya masomo. Pia, ili kuthibitisha matokeo ya kifaa cha ANOVA-njia moja, kifaa cha *t-test* huru sampuli mbili kilitumiwa. Jedwali 5 linawasilisha matokeo ya mchanganuo husika.

**Jedwali 5: Mielekeo ya Wanafunzi kwa Misingi ya Michepuo ya Masomo**

| **ANOVA-njia moja** | **F=1.64** | **Thamani ya uwezekano ya *p* 0.2031 (*Probability value*)** |
|---|---|---|
| *t-test* huru sampuli mbili | Wastani (Sanaa)=84.32<br>Thamani ya *t* (thamani ya *p*)=1.2787 | (Sayansi)=86.25. tofauti=1.93<br>(0.2031) |

Chanzo: *SPSS* toleo 23, (2017); Data Iliyochanganuliwa

Katika Jedwali 5, matokeo ya mchanganuo wa ANOVA-njia moja yalidhihirisha kuwa utofauti wa alama za wastani baina ya michepuo ya sanaa na sayansi, yenye thamani ya uwezekano ya *p* 0.2031 ilikuwa zaidi ya kizidishi cha alfa 0.05. Hivyo, kwa sababu thamani ya uwezekano ya *p* 0.2031 ilizidi kizidishi cha alfa 0.05, ilidhihirisha kuwa hakuna tofauti ya mielekeo baina ya michepuo yote miwili kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano. Utofauti huu ulikuwa finyu, hivyo ulidhihirisha kuwa michepuo ya masomo haikuathiri mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano.


Kwa kuthibitisha matokeo ya ANOVA-njia moja, kifaa cha *t-test* huru sampuli mbili kilitumiwa kukokotoa thamani ya uwezekano ya *p* hali ambayo matokeo yenye mfanano yalidhihirika. Matokeo ya alama ya wastani ya wanafunzi wa mchepuo wa sanaa yalikuwa 84.32 na sayansi 86.25; huku zikizalisha alama wastani ya utofauti kuwa 1.93, yenye thamani ya uwezekano ya *p* 0.2031. Kwa kuwa thamani ya uwezekano ya *p* ni zaidi ya kizidishi cha alfa 0.05, mielekeo ya makundi yote mawili ilionekana kuwa sawa. Hata hivyo, wanafunzi wa mchepuo wa sayansi walidhihirisha alama ya wastani ya juu zaidi ya wanafunzi wa mchepuo wa sanaa. **Wanafunzi wa sayansi huenda walidhihirisha mielekeo yenye uchanya zaidi kwa sababu wanakuwa na upungufu wa maarifa ya**

**mawasiliano na wanaona ni muhimu kwao, ndiposa wenzao wa sanaa wanawafananisha na *machine talkers*, yaani "wanaojua kuzungumza na mashine peke yake." *Hivyo, wao na mashine peke yao.*** Utafiti huu unakinzana na matokeo ya utafiti wa Rad (2009) alioufanya katika Chuo Kikuu Kerman Azad, Saudi Arabia na aliyegundua kuwa kigeu cha michepuo ya masomo kiliathiri mielekeo ya wanafunzi wa sanaa waliokuwa na mielekeo chanya zaidi wanapolinganishwa na wa sayansi kuhusu lugha ya Kiingereza kama lugha ya kigeni kwa misingi ya imani waliyokuwa nayo kuihusu. Alihitimisha kwamba tofauti hii ya kimielekeo ilisababishwa na tofauti ya mitaala baina ya michepuo yote miwili.

Kwa mujibu wa Ajzen na Fishbein (1980) binadamu hutathmini vitendo anavyofanya vingemnufaisha na ikitokea hivyo, basi huwa na mielekeo chanya kuhusu vitendo husika. Hivyo, ikiwa havimnufaishi huwa na mielekeo hasi kuvihusu. Kwa hali hii, ni wazi **wanafunzi wa mchepuo wa sayansi waliona umuhimu wa somo la Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika utoaji wa huduma, ndiposa mielekeo yao ilidhihirika kuwa ya juu ikilinganishwa na ya wanafunzi wa mchepuo wa sanaa.** Makundi haya yalipoulizwa kama walikubaliana na maoni kuwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili ziliwafaa zaidi wanafunzi wanaosoma kozi zenye mketo wa sanaa au sayansi, wanafunzi wengi wa mchepuo wa sayansi walipinga. Katika majibu yao walisema "wanahitaji Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili zaidi kwa sababu wanajihisi kuwa na upungufu wa kimawasiliano zaidi ya wanafunzi wa sanaa, hivyo walihitaji kuchonga stadi za kimawasiliano".

Waaidha, walikuwa na maoni kuwa wanafunzi wote wanahitaji Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili kwa sababu maarifa husika yangewasaidia kuwasiliana kwa ufasaha zaidi ikiwa wangetumwa uwandani kutoa huduma kwa umma. Kuhusu hili inasemekana "mielekeo ya mhusika kuhusu kitendo fulani hubeba hisia za mtu juu ya matokeo tarajiwa … " (Lord, 1997). Matokeo tarajiwa kwa hali hii ni faida ambayo wanafunzi wa sayansi wanatarajia kupata baada ya kuanzishwa kwa ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya.

Kwa muhtasari, mielekeo ya michepuo ya sanaa na sayansi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano inaweza kuwasilishwa katika Mchoro 3.





**Mchoro 3: Alama za Wastani za Mielekeo ya Sanaa na Sayansi Kimichepuo**

Mchoro 3 unaonesha kuwa wanafunzi wa mchepuo wa sanaa walidhihirisha alama za wastani za mielekeo 84.32, ilhali wa sayansi walikuwa na alama 86.25. Hii ilionesha kuwa mielekeo ya wanafunzi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano ilikuwa chanya na haikuathiriwa na michepuo ya masomo. Fauka ya haya, ilidhihirisha kuwa wanafunzi wa mchepuo wa sayansi walipendelea matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano zaidi ya mchepuo wa sanaa.

**Misimamo ya Wanafunzi wa Taasisi za Kiufundi za Kitaifa kuhusu Ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili na Visababishi vya Mielekeo Chanya au Hasi**

"Mielekeo hudhihirisha hisia za kesho na fikra kuhusu tunachokihisi na kukifikiria" (Horowitz & Bordens, 1995). Hivyo, mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa ni muhimu kuhusu ukubalifu wa ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Kwa hali hii, swali la 16 (***Toa maoni yako kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa***), lililenga kupima mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya na kuihusisha na kauli andamizi ya 6 ya Likert (***Ujifunzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili unavutia***).

Katika swali la 16, wasailiwa walitakiwa kutoa maoni yao kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya. Walipewa vibadala vinne kuitikia ambavyo ni: napenda kufundishwa sana, napenda kiasi, sipendi kufundishwa, na sipendi kufundishwa hata kidogo. Matokeo ya miitikio ya swali hili yaliwasilishwa katika Mchoro 4 unaofuata.




**Mchoro 4: Misimamo ya Wanafunzi kuhusuUfundishwaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili**

Matokeo ya miitikio ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi katika Mchoro 4 yanadhihirisha kuwa wanafunzi 78 (54.93%) walipendelea kufundishwa sana Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Waliopenda kufundishwa kiasi walikuwa 53 (37.32%). Hivyo, kwa ujumla, waliopenda kufundishwa sana na kiasi walikuwa 131 (92.25%). Hii ni asilimia ya juu sana ikilinganishwa na waliosema hawapendi kufundishwa. Sababu walizotoa za mielekeo chanya na kupendelea kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili ni pamoja na:

(i) Zitatuwezesha kuwasiliana ipasavyo
(ii) Zitatuwezesha kutoa huduma kwa umma kwa njia inayofaa
(iii) Zitatupunguzia upungufu wa lugha sanifu
(iv) Zitatuwezesha kuelewana na wenzetu na tunaoenda kuwahudumia
(v) Ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiingereza na Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili utawekwa kwa kiwango sawa
(vi) Kupanua misamiati ya kiufundi kwa Kiswahili

Sababu hizi ni dhihirisho tosha kwamba wanafunzi wa taasisi za kiufundi tayari waliridhia kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Asilimia 92.25 ya wanafunzi walioridhia ni ya juu mno; hivyo ni muhimu kuwafundisha Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Kwa upande mwingine, wanafunzi 9 (6.34%) walionyesha kutoridhia kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Waliosema hawataki kufundishwa hata kidogo walikuwa 2 (1.41%). Kwa ujumla, wanafunzi 11 (7.75%) hawakupenda kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Hii ni asilimia ndogo mno ikilinganishwa na waliopendelea kufundishwa ambayo ni 131 (92.25%).

Matokeo ya swali la 16, yakilinganishwa na matokeo ya kauli andamizi ya Likert ya 6 (*Ujifunzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili unavutia*), yalionekana kudhihirisha muoano. Hii ilidhihirishwa na jinsi

wasailiwa walivyoitikia kauli hii. Wanafunzi 127 (89.43%) walisema ujifunzaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili unavutia. Hivyo, kwa maoni ya utafiti huu, walionyesha wangependelea kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Asilimia hii ilioana na walioridhia kuwa wangependa kufundishwa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili ambayo ni 131 (92.25%). Tofauti iliyopo baina ya walioridhia kufundishwa katika matokeo ya swali la 16 (92.25%) na waliovutiwa na Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili kulingana na matokeo ya kauli andamizi ya Likert ya 6, ambao ni asilimia 89.43 ni finyu. Kwa hali hii, matokeo ya swali la 16 na matokeo ya kauli andamizi ya Likert ya 6 yalionekana kuoana. Hili ni dhihirisho la utoaji wa matokeo ya kutegemewa ya kifaa cha Likert katika utafiti huu. Kimsingi, matokeo yake ni kuwa mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya ni chanya kuhusu ufundishaji wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili. Hata hivyo, waliokuwa na mielekeo hasi waliona ***lugha ambayo ingetumiwa kuwasilisha stadi husika ni ngumu, Kiswahili hakina umuhimu wowote na Kiswahili kifundishwe katika viwango vya chini kwani ni katika kiwango hicho kinafaa.***

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Utafiti huu ulichunguza mambo mbalimbali kuhusu mielekeo ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa nchini Kenya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano. Ni wazi kuwa matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa wanafunzi wa taasisi hizi wana mielekeo chanya kuhusu wao kufundishwa stadi za mawasiliano kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Fauka ya haya, wao waliridhia kuwa pana pengo kubwa la utoaji wa huduma ambalo linahitaji kuzibwa kupitia ufundishaji wa stadi za mawasiliano katika taasisi za kiufundi nchini. Hili lilidhihirishwa wazi na wanafunzi wa sayansi kupitia wao kujiona wamepungukiwa katika stadi za mawasiliano katika lugha ya Kiswahili. Jambo lingine la kutilia maanani ni kuwa miongoni mwa taasisi zilizoshirikishwa katika utafiti huu, ni mbili tu (Kabete na Kisii) ambazo zilikuwa na wanafunzi wanne (4) wenye mielekeo hasi (asilimia 2.82); ambao ni uchanya wa chini. Wanafunzi wengine 138 (asilimia 97.18) katika taasisi nyingine (Kenya Coast, Meru na Eldoret) walidhihirisha mielekeo chanya na hakukuwa na wanafunzi wenye mielekeo ya ukatikati au uvuguvugu. Hili lilikuwa wazi kuwa wanafunzi husika walikuwa wanajua umuhimu wa Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika utoaji wa huduma uwandani.

**Mapendekezo:** Kutokana na madhumuni yaliyokuwa yakichunguza mielekeo ya wanafunzi wa sanaa na sayansi kuhusu matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za mawasiliano katika taasisi za kiufundi za kitaifa, makundi yote mawili yalikuwa na mielekeo chanya. Japo wanafunzi wa sanaa walidhihirisha mielekeo chanya ya chini, wakilinganishwa na wa sayansi. Waliona Stadi za mawasiliano kwa Kiswahili zingepambana na *Sheng* miongoni mwa vijana katika taasisi husika. Pia, zingepunguza athari za lugha mama, matamshi mabovu na kupunguza upungufu wa usikilizaji mbovu na kunoa makali ya stadi za kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika. Ni kutokana na haya, utafiti huu unapendekeza Taasisi ya Ukuzaji Mitaala (KICD) na Wizara ya Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia (MOHEST) washirikishe Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili katika mtaala wa taasisi za kiufundi za kitaifa na taasisi nyingine za kiufundi nchini. Hata hivyo, kama kianzio wanaweza kushirikisha kiwango cha astashahada. Kwa kushadidia haya, ni wazi kuwa kuna ukuruba mkubwa baina ya Stadi za Mawasiliano kwa Kiswahili na utoaji wa huduma nyanjani. Ni kutokana na haya, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusiana na uhusiano tajwa. Aidha, ni muhimu kuchunguza uhusiano uliopo baina ya maendeleo na stadi za mawasiliano katika lugha za Kiswahili na Kiingereza, huku ulinganishi ukichunguzwa. Vilevile, uchunguzi unaweza kufanywa wa kimielekeo ya mafuzu walio nyanjani kuhusu ufundishaji wa stadi za mawasiliano kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Pia, pana haja ya kuangalia upya mtaala wa elimu ya taasisi za kiufundi ili kushirikisha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika taasisi husika (Kavoi, 2023).

**MAREJELEO**

Ajzen, I., & Fishbein, M. (1980). *Understanding Attitudes and Predicting Social Behaviour*. Prentice Hall Inc.

Al-Bizrah, A. N., Tarique, N. M., & Arain, F. R. (2016). *Students' Attitude towards Communication Skills Training among Female Medical Students in Taif University*. http://www.skyjournals.Org/SJMMS

Alhmali, R. J. (2007). *Student Attitudes in the Context of Curriculum in Libyan Education in Middle and High Schools* (Doctorial dissertation, University of Glasgow, Scotland, United Kingdom). http://theses.gla.ac.uk /61/1/Rajab_Thesis.pdf

Alotaibi, F. S., & Alsaeedi, A. (2016). *Attitudes of Medical Students towards Communication Skills Learning in Western Saud Arabia*. http://www.doi:10.15537 /smj2016.714331

Anvik, T., Gude, T., Grimstad, H., Baerheim, A., Fasmer, O. B., Hjortdahl, P., & Vaglum, P. (2007). Assessing medical students' attitudes towards learning communication skills – Which components of attitudes do we measure? *BMC Medical Education*, *7*(4). http://www.biomedcentral.com/1472-6920/7/4

Eagly, A. H., & Chaiken, S. (1993). *The Psychology of Attitudes*. Harcourt, Brace, Javanovich.

Fazel, I., & Aghamolaei, T. (2011). *Attitudes towards Learning Communication Skills among Medical Students of a University in Iran*. http:// acta. tums.ac.ir/index.php/ acta/ article/download/3807/3782

Gardner, R., & Lambert, W. (1972). *Attitudes and Motivation in Second Language Learning*. Newbury House.

Horowitz, I. A., & Bordens, K. S. (1995). *Social Psychology*. Mayfield Publishing Company.

Karin, S., Ragnhild, E. B., Ingunn, B., & Sofia, K. S. (2017). *Factors associated with pharmacy students' Attitude towards Learning Communication Skills: A study among Nordic Pharmacy Students.* https://brage.bibsys.no/ xmlui/bitstream/handle/11250 /2495030

Katz, D. (1960). The Functional Approach to the study of Attitudes, in *Public Opinion Quarterly*, 24, 163 - 204.

Kavoi, J. M. (2023). Maoni ya wanafunzi wa taasisi za kiufundi za kitaifa kuhusu nafasi ya Kiswahili katika elimu ya ufundi nchini Kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, *2*(1), 84-94. https://doi.org/10.51317/eajk.v2i1.329

Kombo, D., & Tromp, D. L. (2006). *Theses and Proposal Writing*. Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology*. New Age Publishers.

Lightbown, M. P., & Spada, N. (1993). *How Languages are Learned*. Oxford University Press.

Lord, C. G. (1997). *Social Psychology*. Holt Rinehart & Winston.

Lumma-Sellenthin, A. (2012). Students' attitude towards learning communication skills: correlating attitudes, demographic and meta-cognitive variables. *International Journal of Medical Education*, 3, 201-208. https://doi:10.5116/ijme.5066.cef9

Mcleod, S. A. (2008). Likert Scale: Medical student attitudes to a learning communication skills teaching program. http://www.simplypsychology. org/likert-scale.html

Mills, S. (1998). *Oral Communication*. McGraw–Hill.

Mohochi, E. (2005). *Mielekeo ya Wanafunzi kuhusu Lugha ya Kiswahili na Athari zake katika Matokeo ya Mtihani wa Kiswahili wa Kidato cha Nne katika Mikoa ya Pwani na Nyanza, Kenya*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu). Chuo Kikuu cha Egerton, Kitivo cha Sanaa Sayansi Jamii, Njoro, Kenya.

Neupane, M., Neupane, H., & Adhikari, A. (2012). *Attitude towards Learning Communication Skills in Medical Students of Chitwan Medical College, Chitwan, Nepal.* http://www.med-ed-online.org

Nyandwaro, K. L. (2015). *Mielekeo ya Wafanyakazi kuhusu Kiswahili kama Lugha Rasmi katika Wizara za Serikali Nchini Kenya: Mintarafu, Kaunti ya Kisii*. (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kitivo cha Sanaa na Sayansi Jamii, Nairobi, Kenya.

Oso, W. Y., & Onen, D. (2005). *A General Guide to Writing Research Proposal and Report: A Handbook for Beginning Researchers.* Jomo Kenyatta Foundation.

Padwick, A. (2010). *Attitudes towards English and Varieties of English in Globalizing India*. (Master's thesis) University of Groningen, New Castle, England.

http://scripties.let.eldoc.ub.rug.nl/FILES/root/Master/Doorstroomasters/Eurocultare/2009/a.m.j.padwick/MA-2802445-A.Padwick.pdf

Rad, F. (2009). Evaluation of English students' beliefs about English as a forein language: A case of Kerman Azad University. *International Conference ICT for Language.* (3rd ed.) http://pixel.online.org/ICT4LL2010/common/download/preedings_ pdf/SLA- Fatehi_Rad.pdf

Rees, C., & Sheard, C. (2002). The relationship between medical students' attitudes towards communication skills learning and their demographic and education-related characteristics. *Medical Education*, *36*(11). https://doi.org/10.1046/j.1365-2923.2002.01333.x

Rees, C., Sheard, C., & Davies, S. (2002). The development of a scale to measure medicalstudents' attitudes towads communication skills learning: The communition skills attitude scale (CSAS). In *Medical Education, 36*(4), 141-147. http://dx.doi.org/10.1046/j.1365-2923.2002.01072.x

Richa, R., Yashoda, I., & Puranik. (2017). *Dental Students' Attitude towards Learning Communication Skills in Bengaluru City, India.* https://www.jiaphd.org/text.osp?2016/14/3/327/187174

Trifkovc, K. C., Lorber, M., Denn, M., Denieffe, S., & Gonc, V. (2017). *Attitudes of Nursing Students towards Learning Communication Skills*. http://dx.doi.org/10.5772/67622

Wanjala, F. S., & Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili: Kwa Wanafunzi, Walifunzi na Walimu*. Serengeti Educational Publishers.